JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI

**TUME YA TAIFA YA MIPANGO**

# TAARIFA MUHIMU

DIRA 2050

# MUUNDO WA DIRA 2050



# MISINGI YA DIRA 2050

- **Utawala Bora:** Kuzingatia misingi ya katiba, utawala wa sheria, haki za binadamu, uwazi, uwajibikaji na ushirikishwaji ili kuimarisha taasisi, kuboresha utoaji wa huduma za umma na kujenga imani ya wananchi kwa Serikali.

- **Amani, Usalama na Utulivu:** Kulinda umoja wa kitaifa, mshikamano wa kijamii na mazingira salama kama masharti muhimu ya kuvutia uwekezaji na kufanikisha maendeleo jumuishi, endelevu na ya muda mrefu

## NGUZO ZA DIRA 2050




# Nguzo ya Kwanza:

**Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani**

---

- Uchumijumla Tulivu na unaotabirika.
- Mfumo Endelevu wa Kibajeti.
- Vyanzo Anuai na Bunifu wa Kibajeti
- Mazingira wezeshi ya biashara na Uwekezaji
- Sekta binafsi imara.
- Ushiriki wa kimkakati katika ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

## NGUZO ZA DIRA 2050



# Nguzo ya Pili:

## Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii

- Jamii iliyoelimika, yenye ujuzi na inayopenda kujifunza.
- Jamii yenye afya.
- Hifadhi ya Jamii.
- Makazi Bora ya Gharama Nafuu.
- Nguvu kazi yenye Ujuzi na Ari.
- Jamii yenye Umoja, mshikamano na Inayowajibika.

## NGUZO ZA DIRA 2050

# Nguzo ya Tatu:



**Uadilifu wa Mazingira na Uhimilivu dhidi ya Mabadiliko ya Tabianchi**

---

- Uhifadhi wa Bioanuai
- Uhifadhi wa Ardhioevu na Vyanzo vya Maji.
- Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira
- Usimamizi Madhubuti wa Ardhi.
- Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi

# MALENGO, SHABAHA, SEKTA ZA MAGEUZI NA VICHOCHEO VYA DIRA 2050

## 01 Usafirishaji Fungamanishi

Kuendeleza mtandao fungamanishi wa usafirishaji na uchukuzi wenye mfumo shindani wa njia mbalimbali za usafiri pamoja na miundombinu ya kisasa inayoendana na vipaumbele vya maendeleo ya nchi



## 02 Nishati


Kujenga mfumo wa nishati unaotegemewa, unaomudu gharama na ulio safi; na kuifanya Tanzania kuwa msafirishaji wa nishati kwenda nje ifikapo mwaka 2050.



# MALENGO, SHABAHA, SEKTA ZA MAGEUZI NA VICHOCHEO VYA DIRA 2050

## 03 Sayansi na Teknolojia

Kuongeza tija kupitia teknolojia za kisasa na mifumo imara ya ubunifu.



## 04 Utafiti na Maendeleo

Kuimarisha mfumo wa kitaifa wa ubunifu kwa kuelekeza angalau asilimia 1 ya Pato la Taifa (GDP) katika utafiti na maendeleo.



## 05 Mageuzi ya Kidijitali

Kupanua uelewa na upatikanaji wa huduma za kidijitali, kuongeza ufanisi wa Serikali na kuwezesha matumizi ya kibiashara ya takwimu.



# MALENGO MAKUU NA SHABAHA DIRA 2050

## LENGO LA 1

**Uchumi wa kipato cha kati ngazi ya juu, ulio mseto, himilivu, jumuishi na shindani.**

***Shabaha:***

- Uchumi wa dola za Marekani trilioni 1 Wastani wa pato la mtu mmoja wa dola za Marekani 7,000 kwa mwaka.
- Kutokomeza umaskini uliokithiri kwa makundi yote.
- Kuwa mzalishaji mkuu wa chakula barani Afrika na miongoni mwa nchi 10 bora duniani.

# MALENGO MAKUU NA SHABAHA DIRA 2050

## LENGO LA 2

**Maisha bora na ustawi kwa wote.**

***Shabaha:***

- Mtanzania anaishi kwa wastani wa miaka 75, akifurahia maisha bora na afya njema..
- Watoto wote wa kike na wa kiume wanapata malezi na makuzi bora ya utotoni.
- Kutokomeza vifo vya wajawazito, watoto wachanga na watoto wenye umri chini miaka mitano.
- Huduma bora za afya kwa wote.
- Mfumo bora na jumuishi wa elimu na mafunzo katika ngazi zote.

# MALENGO MAKUU NA SHABAHA

## LENGO LA 2

### Kuboresha ubora wa maisha na ustawi kwa wote

***Shabaha:***

- Upatikanaji sawa wa elimu bora ya awali na msingi.
- Angalau asilimia 25 ya wananchi wanapata elimu ya juu
- Hifadhi ya jamii kwa wote.
- Upatikanaji sawia wa maji safi na salama, huduma za usafi wa mazingira na nishati safi.
- Angalau asilimia 50 ya watanzania wana ajira zenye staha sekta rasmi zenye staha.
- Matumizi ya umeme kufikia kilowati saa 3,000 kwa mtu kwa mwaka.
- Tanzania kuwa kinara Afrika na miongoni mwa nchi 10 bora duniani katika kupunguza pengo la kijinsia kwa asilimia 85.

# MALENGO MAKUU NA SHABAHA DIRA 2050

## LENGO LA 3

**Taifa linalohifadhi na kutumia rasilimali za asili kwa ufanisi, uendelevu na tija, na linalostahimili mabadiliko ya tabianchi.**

***Shabaha:***

- Kuwa na viwango vya juu vya uhifadhi wa mazingira na uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi na kuifanya Tanzania kuwa kati ya nchi kumi bora barani Afrika

# MALENGO MAKUU NA SHABAHA DIRA 2050

## LENGO LA 4

**Jamii yenye umahiri na ujuzi wa kutumia teknolojia za kidijitalikatika kuchochea ubunifu na kuongeza ushindani wake kimataifa.**

***Shabaha:***

- Jamii yenye umahiri wa kidijitali ambapo angalau asilimia 70 ya wananchi wawe na ujuzi wa kidijitali.
- Zaidi ya asilimia 80 ya huduma za Serikali zipatikana kupitia mifumo ya kidijitali salama na jumuishi.

# SEKTA ZA MAGEUZI

- Kilimo
- Utalii
- Uzalishaji Viwandani
- Ujenzi na Milki
- Madini
- Uchumi wa Buluu
- michezo na ubunifu
- Sekta ya fedha
- Sekta ya Huduma

**www.planning.go.tz**

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**
**Tume ya Taifa ya Mipango**
**1 Mtaa wa Kambarage 41104 Tambukareli Jengo la Kambarage,**
**postikodi 40477, Gorofa ya tisa(9), S.L.P 1324, DODOMA**